

BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



Dodoma

21 Agosti 2023

NOTISI YA KUFUTA USAJILI WA VYUO

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129 pamoja na Marekebisho Madogo Na. 6 ya Mwaka 2021, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Moja ya jukumu la Baraza chini ya Kifungu cha 5 (1) (f) ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini yanakidhi vigezo na ubora katika muda wote wa mafunzo.

Kwa kuzingatia dhamana hiyo, Baraza linakusudia kufuta usajili kwa vyuo vilivyoshindwa kutoa elimu inayokidhi vigezo vya elimu ya ufundi nchini. Hivyo, Baraza linatoa notisi ya siku 14 ya kusudio la kufuta usajili wa vyuo vifuatavyo:

1. Institute of Lands Dar es Salaam;
2. Institute of Social Work Mwanza Campus;
3. The Lake Tanganyika Zone College – Sumbawanga;
4. Rukwa College of Health Sciences – Sumbawanga;
5. Tanzania Aviation College – Arusha;
6. Tanzania Aviation College - Dar es Salaam; na
7. Tanzania Aviation College – Mwanza.

Aidha, wamiliki wa vyuo tajwa wanatakiwa kuwasiliana na Baraza ndani ya siku 14 toka tarehe ya notisi hii, yaani kuanzia leo tarehe 17 Agosti 2023.

**IMETOLEWA NA OFISI YA KATIBU MTENDAJI
NACTVET**

**Barabara ya Mwangosi, 41110 Kilimani,
P. O. Box 17007,
DODOMA.
Barua pepe: info@nacte.go.tz**